

## HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA

Tarehe 20/06/2023



### ILANI YA KUSUDIO LA KUTUNGA SHERIA NDOGO

Halmashauri ya Wilaya ya Tandahimba inawatangazia wananchi wote wa Tandahimba kuwa inakusudia kutunga Sheria Ndogo zifuatazo kutokana na mamlaka iliyopewa chini ya kifungu cha 89(1) cha Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya) suraya 287 ya mwaka 2002 na Sheria zingine za nchi.

1. SHERIA NDOGO YA (ADA NA USHURU) YA HALMASHAURI YA TANDAHIMBA YA MWAKA 2023
2. SHERIA NDOGO YA (USHURU WA HUDUMA) YA HALMASHAURI YA TANDAHIMBA YA MWAKA 2023
3. SHERIA NDOGO YA (BODI YA MFUKO WA ELIMU) YA HALMASHAURI YA TANDAHIMBA YA MWAKA 2023
4. SHERIA NDOGO YA (AFYA NA USAFI WA MAZINGIRA) YA HALMASHAURI YA TANDAHIMBA YA MWAKA 2023
5. SHERIA NDOGO YA (UVUNAJI WA MAJI YA MVUA) ZA HALMASHAURI YA TANDAHIMBA YA MWAKA 2023
6. SHERIA NDOGO YA (UUZAJI NA UNUNUZI WA KOROSHO KARANGA) YA HALMASHAURI YA TANDAHIMBA 2023
7. SHERIA NDOGO YA (NYUMBA ZA KULALA WAGENI) YA HALMASHAURI YA TANDAHIMBA YA MWAKA 2023
8. SHERIA NDOGO YA (ADA YA VIBALI VYA UTAMADUNI NA BURUDANI) HALMASHAURI YA TANDAHIMBA ZA 2023
9. SHERIA NDOGO YA (MAHUDHURIO YA LAZIMA NA UPATIKANAJI WA CHAKULA MASHULENI) ZA YA TANDAHIMBA 2023
10. SHERIA NDOGO YA (USHURU WA MAZAO MCHANGANYIKO) YA HALMASHAURI YA TANDAHIMBA YA MWAKA 2023

Wananchi wanaweza kushiriki katika kutunga Sheria Ndogo hizi kwa kutoa pingamizi, ushauri au hoja. Rasimu za Sheria husika zimewekwa kwenye ofisi za kata zote za Halmashauri kwaajili ya ukaguzi nyakati na siku za kazi kuanzia tarehe 25/06/2023. Wananchi watakaotaka kurudufu nakala za rasimu za sheria hizo watafanya hivyo kwa gharama zao wenyewe.

Aidha Halmashauri inawataarifu wananchi kuwa pingamizi au hoja zozote kuhusu rasimu za Sheria Ndogo ziwe zimewasilishwa kwenye ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ndani ya siku Ishirini na Moja (21) kuanzia tarehe ya tangazo hili au kwenye ofisi ya Mtendaji wa Kata iliyokaribu.

A handwritten signature in black ink, appearing to read 'Robert Mwanawima'.

**ROBERT MWANAWIMA**  
**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA TANDAHIMBA**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)  
S. L. P. Box 03  
TANDAHIMBA